

Huduma zote za serikali na za jamii zinapaswa:

- kukufanya ujisikie kukaribishwa
- kukuchukulia kwa heshima
- kukuchukulia kwa usawa na kila mtu mwingine
- kuwa na ufahamu wa tamaduni mbalimbali
- kukusaidia kuelewa haki zako.

Unaruhusiwa kulalamika kuhusu mtoa huduma.

Mchunguzi Mkuu wa NSW (The NSW Ombudsman)

Tuko hapa kusaidia kila mtu katika NSW.

Tunataka kila mtu atendewe haki.

Huduma zetu zinatolewa bure.

Wasiliana Nasi



Piga simu 02 9286 1000

Kupiga simu kwa bure 1800 451 524

nje ya maeneo ya Sydney mjini
- gharama zinaweza kutozwa kwa simu za mkononi.



nswombo@ombo.nsw.gov.au



Huduma ya Kitaifa ya Wasiosikia 133 677



Mkalimani

Hatua ya 1: Piga simu TIS 131 450

Hatua ya 2: Uliza kuongea na NSW

Ombudsman - 9286 1000



www.ombo.nsw.gov.au

ISBN: 978-1-925885-75-0



Je, una tatizo na huduma ya Serikali ya NSW au huduma ya jamii?

Je umewahi kujaribu kutoa malalamiko. Lakini Haikusaidia.



Mchunguzi Mkuu wa NSW (NSW Ombudsman) anaweza kukusaidia.



Tunaweza kukusaidia:

- kutuma barua kwa mtoa huduma
- kupata mtu sahihi wa kuwasiliana
- kusema matokeo unayotaka kutokana malalamiko uliyonayo.

Tunaweza:

- kukuuliza kuleta karatasi zozote ulizo nazo kuhusu tatizo, kama barua ulizoandika kwa mtoa huduma au barua ambazo mtoa huduma alikuandikia
- kuzungumza na mtoa huduma ambaye una tatizo naye
- kuongea na watu wengine ambao wamekusaidia.



Unadhani ulichukuliwa katika hali isiyo ya haki?



Je, umewahi kujaribu kupata msaada, lakini haukuweza:

- kutatua tatizo
- kupata habari zaidi
- kutafuta kujua kuhusu haki zako.



Wafanyakazi hawakuwa wa msaada, au

- walikuwa wajeuri na hawakukuheshimu
- haukuwa na taarifa katika lugha yako
- hakukuwa na mkalimani.

Watu wengine wanaweza kuwa na tatizo sawa na wewe. Tunafanya kazi na watoa huduma ili kufanya huduma kuwa bora kwa kila mtu.